

HISTORIA FUPI YA WILAYA YA CHATO

Chato ni mojawapo ya Wilaya tano za Mkoa wa Geita na ilianzishwa rasmi Julai 2006 kutokana na kugawanywa kwa Wilaya ya Biharamulo. Wilaya ya Chato ina Halmashauri moja yaani Halmashauri ya Wilaya ya Chato iliyoanzishwa rasmi Julai, 2007.

MIPAKA NA ENEO LA WILAYA

Wilaya ya Chato ipo Kaskazini Magharibi mwa Tanzania kati ya Latitudo 2⁰ 15' hadi 3⁰ 15' Kusini mwa Ikweta na Longitudo 31⁰ hadi 32⁰ Mashariki ya Greenwich. Wilaya inapakana na Wilaya ya Muleba Kwa upande wa Kaskazini, Wilaya ya Bukombe kwa upande wa Kusini, Wilaya ya Biharamulo kwa upande wa Magharibi na Wilaya ya Geita kwa upande wa Mashariki. Wilaya ina eneo la kilometa za mraba 3,572 na iko kwenye mwinuko wa kati ya meta 1,135 hadi 1,410 kutoka usawa wa bahari.

IDADI YA WATU

Kutokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ilikuwa na idadi ya watu 365,127 ambapo kati ya hao 181,368 ni Wanaume na 183,759 ni Wanawake. Idadi ya kaya ni 60,855 sawa na wastani wa watu 6 kwa kaya. Wilaya ina watu wenye uwezo wa kufanya kazi wapato 175,261 sawa na asilimia 48 ya wakazi wote. Hadi kufikia 31 Desemba, 2017 Wilaya inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao 420,191 wanaume ni 208,720 na wanawake ni 211,471 (***Chanzo cha taarifa NBS***)

UTAWALA

Kiutawala Wilaya ya Chato imegawanyika katika Tarafa 5 za Buzirayombo, Bwanga, Buseresere, Kachwamba na Nyamirembe. Kuna Kata 23 zenye Vijiji 115 na Vitongoji 599. Makao Makuu ya Wilaya ni Chato. Wilaya ina jimbo moja la uchaguzi, Madiwani 32 ambapo kati yao 23 ni wa kuchaguliwa kwenye Kata na 8 ni wanawake kupitia viti maalum na Mhe. Mbunge 1.